MSc Environment and Sustainable Development | OVERDUE Learning Alliance 2022-23

# CHUNGU KIENDELEE KUPIKA

Mfuko wa mikopo ya kijamii wenye lengo la kuboresha hali ya vyoo na usafi wa mazingira

**Waandishi**
Lucy DiSanto
Delbert Lim
Kinanti Aldhia Naura
Kome Mallam-Obi
Md Fahim Azraf Khan
Warda Reggane
Radhika Mehta
Ka Hei Chan
Zhitao Chen



**Kielelezo cha 1:** Karibu sana kwa Mazoezi, Mwanza, 2023. Mkopo wa Picha: Warda Reggane

## MUHTASARI WA SERA

### Mambo muhimu

- Ili kuhahakisha jamii inakuwa na mafanikio ya muda mrefu ya kuendeleza juhudi zake kuanzia ngazi ya chini kwa kutoa fedha kwa kukopesha na kuzungusha ili iweze kuwanufaisha wanajamii wengi zaidi kuendana na mahitaji ya yao, ni muhimu kuhakikisha uwiano wa mambo matatu muhimu ambayo ni: ushirikishwaji wa jamii, uendelevu wa kifedha na muktadha wa eneo husika.

- Ili fedha za mkopo zinazozungushwa ziwe na ufanisi, lazima ziwe na mifumo ya wazi ya usimamizi na uongozi.

- Ili kuwezesha uendelevu wa kifedha, lazima kuwe na aina mbalimbali za ufadhili, za nje na za ndani.

- Kufikia usawa wa usafi wa mazingira inahitaji kuwezesha jamii kupata sehemu ya chaguzi mbalimbali za mambo muhimu kuihusu jamii kupitia mifuko ya fedha.

- Ili mifuko ikuwe, fedha izungushwe na ichangie katika maendeleo ya haki ya kijamii, lazima kuwe na ufadhili wa pamoja unaotokana na ushirikiano wenye nguvu na ushirikiano wa wadau mbalimbali.

## Utangulizi

Kufikia mwaka wa 2050, zaidi ya theluthi mbili ya watu duniani inatarajiwa kuwa mijini, huku wengi wakiishi katika makazi yasiyopangwa na yasiyo rasmi na katika maeneo madogo ya mijini barani Afrika na Asia [1]. Ukuaji huu wa miji unaleta changamoto kadhaa , kwani jamii za kipato cha chini ambazo zinaishi katika makazi yasiyo rasmi mara nyingi huishi katika maeneo hatarishi na yasiyofaa zaidi [2]. Mwanza, jiji la pili kwa ukubwa nchini Tanzania, barani Afrika, pia linakabiliwa na changamoto hizi, ambapo takriban 75% ya wakazi wanaishi katika makazi yasiyopangwa kwenye maeneo yenye miinuko na miamba mwaka 2018. Kwa sababu hiyo, utoaji wa huduma za msingi za usafi wa mazingira unakumbwa na changamoto za kijiografia ya maeneo hayo pia na ukosefu wa miundombinu ya barabara [3]. Zaidi ya hayo, kwa sababu wengi wa kaya hizi zinajumuisha watu wa kipato cha chini wasio na ajira rasmi na umiliki wa makazi, upatikanaji mdogo wa fedha za ufadhili wa mtu binafsi kwa ajili ya vifaa vya choo katika maeneo haya [4]. Hii inaonyesha tofauti kati ya hitaji la huduma ya usafi wa mazingira na upatikanaji wa fedha za ujenzi.

Jukwaa na Mfuko mpya wa uboreshaji wa vyoo na Usafi wa Mazingira wa Jiji la Mwanza (MCSFF) unalenga kukabiliana na changamoto hii kwa kuanzisha mfuko utakaofikiwa na jamii na endelevu kwa ajili ya maendeleo, uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya usafi wa mazingira binafsi (nyumba mojamoja) na ya Jamii . Fedha za kianzio za MCSFF zimepatikana kupitia mfuko wa flexi- fund uliotolewa na mradi wa OVERDUE, huu ni mradi shirikishi wa utafiti unaofanya kazi katika miji saba ya Afrika na unaojumuisha wataalam kutoka Kitengo cha Mipango ya Maendeleo ya Bartlett UCL, Chuo Kikuu cha Ardhi, shirika la (CCI), Kituo cha Utafiti cha Mijini cha Sierra Leone (SLURC). Madhumuni ya mradi huu ni kushughulikia shida ya hali mbaya ya vyoo na usafi wa mazingira katika miji ya Afrika kupitia kukuza uelewa kupitia simulizi na mada kuhusu mila na desturi na miiko iliyopo, , kuchunguza njia za kukabiliana na mazoea ya kila siku, na kusaidia kukuza nafasi za mazungumzo [6].

Njia moja ya kuuendeleza mfuko kama vile MCSFF ni kuona kama "Chungu" (kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo 2) cha fedha ambazo mikopo hutolewa inapohitajika. Lengo ni kuweka vilivyomo ndani ya chungu hiki kikiwa kimejaa na kuchemka wakati wote, ili kiendelee kulisha jamii. “Viungo” kadhaa muhimu vimetambuliwa kuwa muhimu katika “kichocheo cha mafanikio” ili kuhakikisha uendelevu wa mfuko huu na uwezo wake wa kukidhi mahitaji ya kila wakati ya uboreshaji wa usafi wa mazingira jijini Mwanza. Kupitia kazi ya field iliyofanyika Mabatini, Mwanza, na kuunganisha mafunzo kutoka katika muktadha sawa, kanuni (au “viungo”) zilizotambuliwa ambazo lazima ziwe na usawa na ujumuishaji wa Jamii, , uendelevu wa kifedha, na muktadha wa eneo huska.


Muhtasari huu utafafanua umuhimu wa kupata usawa katika kanuni hizi kabla ya kuangazia mikakati inayoweza kutekelezwa ya kuunda suluhisho bora linaloongozwa na jamii ili kukuza usawa wa huduma za usafi wa mazingira jijini Mwanza. Mikakati hii iko katika makundi matatu ya utawala na usimamizi, ufadhili wa mseto (unaotegemea vyanzo mbalimbali bila kutegemea ufadhili kutoka nje), na kutoa wigo wa chaguzi. Mwisho, ni muhimu kuonyeshakwamba ufadhili wa pamoja ambapo wahusika wengi lazima wafanye kazi pamoja na kuchangia kwa ushirikiano kudumisha na kusimamia mfuko ili kutimiza malengo haya.

# 1. MUHTASARI WA UTAFITI NA TATIZO

## 1.1 Tatizo: Ukuaji wa Haraka wa Miji na Usafi wa Mazingira

Jiji la Mwanza liko kwenye mwambao wa Ziwa Victoria, Mwanza ni jiji la milimani linalojulikana kwa miamba yake ya ajabu [4]. Jiografia hii, na miundombinu duni ya barabara, inakuja na changamoto za utoaji huduma kama vile mtandao wa maji taka unakuwa gharama isivyoweza kulipwa na watu wengi [7]. Ukosefu huu wa huduma za vyoo na usafi wa mazingira katika maeneo ya jiji, sambamba na ukuaji wa haraka bilia mpangilio wa makazi yasiyo rasmi , umesababisha uchafuzi wa maji na athari kubwa za kiafya [4]. Katika kukabiliana na changamoto hizo, mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (LVWAT- SAN) kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na UN-Habitat ulizinduliwa kwa lengo la kupanua na uboreshaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini ndani ya Bonde la Ziwa Victoria, ikiwemo Mwanza [8]. Hata hivyo, katika wilaya za Nyamagana na Ilemela, ni 6% na 7% tu ya kaya zinazopata huduma ya bomba la maji taka [9]. Hivyo, ikiwa ni sehemu ya mradi wa LVWATSAN Mwanza, ili kukabiliana na kasi ya ongezeko la watu katika maeneo yenye changamoto, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) imeanza kutekeleza mfumo rahisi wa maji taka (yaani SSS) ili kuunganisha kwenye mfumo wa kawaida wa majitaka wa jiji [5].

Upanuzi wa SSS unahitaji vyoo vilivyoboreshwa ili kuunganishwa kwenye mfumo.




**Kielelezo cha 2:** Mahitaji muhimu kwa mfuko wa akiba endelevu ufanikiwe

Hata hivyo, ukosefu wa vyoo bora katika makazi yasiyo rasmi jijini Mwanza bado ni changamoto kubwa, ambayo haiathiri tu ongezeko la wanafuika wa SSS, lakini pia huongeza ukosefu wa usawa miongoni mwa makundi mbalimbali katika jamii. Pamoja na miundombinu iliyopo katika hali mbaya ambayo mara nyingi ni vigumu kufikiwa, wasiwasi wa usalama hutokea kwa wanawake na wasichana, wakati changamoto kutokana na kutofikiwa huwa mzigo mkubwa kwa wazee na watu wenye ulemavu [10]. Kutokana na changamoto hizi za kiufundi na kifedha, utoaji wa huduma za uboreshaji wa miundombinu ya vyoo na usafi wa mazingira inakuwa kazi ngumu inayohitaji mbinu za kibunifu.


Wakazi wa makazi yasiyopangwa sio tu kwamba wanatengwa na huduma za usafi wa mazingira zinazotolewa na jiji kwa sababu ya ukosefu wa hati miliki rasmi za makazi lakini pia wanakabiliwa na ugumu wa kukidhi mahitaji ya kifedha kutokana na mifumo isiyo rasmi ya kupata mikopo [11]. Hii inamaanisha kuwa mikopo kutoka kwa ufadhili rasmi mara nyingi haipatikani kwa sababu ya ukosefu wa ukadiriaji wa mkopo, ajira rasmi, au sheria zingine za kustahiki. Hii inazuia uwezo wa wakazi kupata fedha zao wenyewe kwa ajili ya kuboresha huduma za vyoo na usafi wa mazingira ambazo kwasasa hzipatikani [12].

## 1.2 Suluhisho: "Chungu" cha Utoaji wa fedha kwa ngazi ya chini kabisa ya jamii


Katika kukabiliana na hali hiyo, mitandao ya vikundi vya akiba vya kijamii vinavyojumuisha wanawake vimekuwa katika ngazi ya kimataifa kama njia ya kupata fedha hasa kwa watu wasikini waishio mijini. Vikundi vya kuweka akiba vimetumiwa na watu maskini wa mijini kama njia ya kuboresha maisha yao. Wao ni mfano wa mbinu ya mifuko ya akiba ya kijamii ambayo imekua njia muhimu ya kuimarisha huduma ya vyoo na usafi wa mazingira katika makazi yasiyo rasmi duniani kote [13-15].

Jijini Mwanza, sehemu kubwa ya vikundi hivi vya kuweka akiba vinasimamiwa Federation, ambayo ipo kama sehemu ya mtandao mpana zaidi wa vikundi vya Federation Tanzania (TUPF) [16]. Mratibu waFederation mkoa wa mwanza , Mary Rubelwa, ameeleza kuwa kuna vikundi 35 vya kuweka akiba mkoani Mwanza, ambapo idadi ya wanaume ni 197 na wanawake ni 483.

Kuwa wanachama wa Federation kunawawezesha Jamii watu maskiniMwanza kupata Mfuko wa akibawa maendeleo (JENGA) ambao unatoa mikopo kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile ununuzi wa ardhi, ujenzi wa nyumba, shughuli za kujiongezea kipato na uendelezaji wa miundombinu. Hata hivyo, akiba ya mfuko wa Jenga haitumiki mara kwa mara kwa miradi ya vyoo na usafi wa Mazingira.utafiti [17] unaonyesha kuwa kuna changamoto za ulipaji, haswa kwa miradi isiyoingiza mapato.




**Kielelezo cha 3:** Mfuko wa akiba unaozunguka, kama suruhisho la changamoto za kifedha




**Kielelezo cha 4:** Mikakati ya kuwezesha chungu kuendelea kupika (Mfuko wa akiba kuendelea kukua)

Kwa kutumia muundo huo unaoongozwa na jamii na kuangazia mafunzo kupitia Mfuko wa JENGA, utaratibu mpya wa ufadhili katika ngazi ya chini unaolenga katika kuboresha miundombinu ya vyoo na usafi wa mazingira umeanzishwa kupitia MCSFF. MCSFF inalenga kufanya kazi kama mfuko unaozunguka (Mchoro 3), ikimaanisha kuwa fedha za kianzio hutumika kwa njia mbili; kwanza kama ndoano ya ufadhili au washiriki zaidi na pili kama njia ya kutoa mikopo ya kwanza ambayo inaporejeshwa itaruhusu ufadhili endelevu na wa kujitegemea kwa muda.[1]

## 1.3 Kichocheo cha Mafanikio: "Viungo"

Tukirejea kwenye viungo vinavyohitajika katika chungu hiki cha ujumuishi wa kijamii, uendelevu wa kifedha, na muktadha wa eneo husika ni wazi kwamba ikitokea kikakosekana kimoja wapo, mfuko utakua katika hatari kubwa ya kushindwa kutimiza malengo. Kwa mfano, ikiwa sheria za uidhinishaji wa mkopo zikakabiliwa na vikwazo vingi, fedha hizi hupoteza kile kinachozitofautisha na aina zingine za mikopo inayotolewa na taasisi za kibenki: yaani, uwezo wa kujumuisha wanufaika ambao kwa njia nyingine hawakujumuishwa, na hivyo kuweka ujumuishaji wa kijamii hatarini. Ikiwa mikopo itatolewa kwa wale walio na uhitaji zaidi bila kujali kulipa au bila viwango vya riba, kunauwezekano kwamba akiba kwenye mfuko ikaisha, na kuhatarisha kanuni endelevu ya kifedha. Mwisho, hata kama mfuko unafanya kazi vizuri na endelevu, kuna hatari kwamba itatumika kufadhili miradi mizuri na ya kuvutia lakini isiyoendana na uhalisia wa maeneo husika. Kwa mfano, kujenga vyoo ambavyo vinahitaji kuunganishiwa kwenye mfumo wa maji taka wakati uwezekano wa kuunganyishwa hauwezekani, au kuweka huduma ya vyoo katika maeneo ambayo italazimika kubomolewa wakati barabara mpya itajengwa. Hii inaweza kuhatarisha malengo makuu ya mfuko.

Kwa kuzingatia kanuni hizi muhimu kila wakati, mikakati mitatu ifuatayo ya "kuhakikisha chungu kuendelea kupika" (iliyoonyeshwa kwenye Mchoro 4) Kilichotengenezwa baada ya tafiti mbalimbali na kushirikiana na wadau mbalimbali jijini Mwanza. Timu yetu ilipata maarifa kutokana na majadiliano na viongozi na wanachama wa Federation, viongozi wa serikali za mitaa, wahandisi wa MWAUWASA, na wakazi wa makazi yasiyo rasmi. Hili ilifanyika kupitia majadiliano ya vikundi, kuzunguka eneo husika,vikao vya mahojiano, na warsha ya mwisho iliyoshirikisha jamii, iliyofanyika kwa kiasi kikubwa katika makazi ya Mabatini.

[1] https://dictionary.cambridge.org/dictionary/english/revolving-fund

## 2. Uchunguzi wa matokeo

### 2.1 Mkakati wa 1 - Usimamizi wa pamoja na uongozi

Ni muhimu kuanzisha na kudumisha muundo wa wazi kwa mifuko ya kijamii [18]. Wakati wa mkutano na wanachama wa vikundi vya kuweka akiba jijini Mwanza, timu yetu ilishuhudia mifano chanya na hasi yautawala, ikieleza jinsi inavyochochea mabadiliko. Kwa mfano, mwanamke mmoja aliondoka kikundi cha kuweka akiba cha Mabatini kwa sababu ya kutoamini uongozi wa kikundi hicho, akieleza kuwa kulikuwa na upendeleo wa jinsi mikopo inavyotolewa na ukosefu wa uwazi. Kundi hilo baadaye lilivunjika kabisa. Mhojiwa mwingine alikuwa mweka hazina wa kikundi cha Tujitume tangu 2021, kikundi cha kuweka akiba huko Mabatini chenye wanaume 7 na wanawake 8. Alikuja akiwa ametayarisha vitabu vyake vya kumbukumbu ambavyo vilionyesha utofauti mkubwa wa mfumo utunzaji mzuri wa kumbukumbu ambao unongeza uwajibikaji na uwazi kama inavyoonekana kwenye Mchoro 5.

Kulingana na mifano iliyotajwa hapo juu, tunaamini kuwa fedha zinazoongozwa na wanajamii haziwezi kufanikiwa bila uaminifu na uwajibikaji, na ambazo zinategemea kwa kiasi fulani usimamizi na utawala dhabiti. Kwa usimamizi shirikishi, tunamaanisha kugawana majukumu na uwajibikaji ili vikundi kama hivi viweze kuepuka mienendo mibaya ya viongozi na kuimasha uhusiano miongoni mwawanakikundi na kuaminiana [19]. Vikundi vinapaswa kuhakikisha kuwa wanachama wanakubaliana kwa pamoja kuhusu mifumo iliyopo na kuwajibishana linapokuja suala la kufuata itifaki [20, 21]. Kwa kutoa nafasi ya kutoa maoni yao na kufanya maamuzi ya pamoja, Mifuko ya kijamii kama vile MCSFF ina fursa ya kuwa suluhisho la kuwezesha na kushirikisha Jamii ambapo wahusika wengi huchangia mfuko wa maendelo ya vyoo na usafi wa Mazingira ili kuwezesha chungu kuendelea kutokota. Kielelezo cha 6 kinaonyesha mchoro wa wadau mbalimbali na majukumu yao katika kujenga MCSFF.

Vipengele vya utawala vinavyohitaji ushirikiano kuanzia mwanzo ni pamoja na: kuweka wazi wajibu na majukumu kwa washiriki wote, kuunda miongozo ya utoaji wa mikopo, kukubaliana juu ya muda na masharti ya urejeshaji wa mikopo, kuweka mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya kufuatilia mtiririko wa fedha, na kudumisha uwazi katika mchakato mzima. Mfano wa Uchunguzi 1 hutoa mfano wa utawala thaabiti katika muktadha sawa.

Mapendekezo haya yanaendana na maoni ya jamii kutoka Mwanza. Wakati wa warsha hiyoiliyofanyika Mabatini, wanajamii walishiriki kwa kutoa mapendekezo ya namna mfuko kama MCSFF unapaswa kusimamiwa pamoja kwa ufanisi zaidi. Wazo la kamati ya Jamii yenye uongozi uliochaguliwa ilipendekezwa, kwa madhumuni ya kuamua jinsi ya kutumia mikopo kutoka kwenye mfuko na kusimamia mchakato wa kurejesha. Ilisisitizwa kuwa uongozi usioegemea upande wowote ni muhimu, ili kuepuka kuegemea upande wowote wa vyama vya siasa pamoja na kuwa na mfumo wa kuchagua uongozi. Zaidi ya hayo, wakazi wengi walijadili hitaji la mifumo ya uwazi uwekeji kumbukumbu na ofisi kwa ajiri ya kuhifadhi nyaraka. (au uwezekano wa kuweka kumbukumbu kidijitali) na pia walionyesha nia ya kutafuta fursa za mafunzo ili kujifunza juu ya usimamizi wa mfuko ili kuongeza ufanisi wa kamati kadri iwezekanavyo.

Pendekezo moja ambalo lililotoka kwenye mazungumzo wakati wa warsha na wajamii lilikuwa ni wazo la kuweka kipaumbele mikopo kwa wenye nyumba. Baadhi ya wakazi walielezea kwamba itakua rahisi mwenye nyumba kulipa na kurejesha mkopo na vyoo vyovyote vilivyojengwa vinaweza kunufaisha kaya nyingi kwa wakati mmoja. Ni muhimu kutambua mapungufu ya pendekezo hili, kwani linaweza kuendeleza bila kukusudia mienendo na ukosefu wa usawa wa jumuiya na inaweza kusababisha ongezeko kubwa la kodi kwa wapangaji. Kwa hivyo ingawa wazo hili litahitaji kuchunguzwa zaidi, mchango huu unaangazia jinsi wanajamii wanaweza kusaidia kubainisha miongozo kuhusu vipengele vya utawala kama vile vigezo. Faida ya kuhakikisha wanajamii ni wasimamizi-wenza wa mfuko na kwamba wanaelewa mahitaji na hali za ndani za mfuko vizuri zaidi kuliko wahusika wengine [22].


GMifuko ya kijamii inapaswa kuleta usawa kati ya mifumo rasmi na ile isiyo rasimi ili kuhakikisha kuwa hauzuiliki kupita kiasi au kuhatarisha kanuni ya ujumuishi za kijamii [23]. Hata hivyo, tunasisitiza kwamba mfuko kama MCSFF lazima uchukue muundo na utawala kwa umakini tangu mwanzo ili kufanikiwa.

**Mfano uchunguzi 1:** Mfuko wa Akiba Mashinani Trust (AMT) ulianzishwa ili kufadhili shirikisho la vikundi vya kuweka akiba ambalo limekuwa likifanya kazi nchini Kenya tangu 2003 [20]. AMT inalenga katika kuhakikisha ushiriki na uwajibikaji ndani ya Jamii za mijini na taasisi za kifedha. Wanafanikisha hili kwa kusimamia kikamilifu programu zao ndani ya vikundi vya kijamii kupitia mikutano, kufanya maamuzi ya pamoja, na uwekaji mzuri wa kumbukumbu. Wanachama wanahusika mara kwa mara katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini miradi na taratibu zote, kuanzia ukusanyaji wa mikopo hadi uendelezaji wa nyumba. Ushiriki mkubwa wa wanachama katika kusimamia taasisi unathibitishwa na matokeo ya mahojiano; 90% ya wanachama walionyesha kuelewa maudhui na umuhimu wa sheria ndogo. Zaidi ya hayo, kujitolea kwa uwazi na uwajibikaji kumesababisha ongezeko la mara kwa mara katika kiwango cha ulipaji, ambacho kilipanda kutoka 76% mwaka wa 2012 hadi 93% mwaka wa 2016 [21].



**Kielelezo cha 5:** Mfano wa kitabu cha kumbukumbu za Akiba kikundi cha Tujituma, Mwanza, Tanzania, 2023.Picha: Lucy Di Santo

**Kielelezo cha 6:** Uwezekano wa wadau kwa Ushirikiano wa MCSFF




### 2.2 Mkakati 2 - Ufadhili Mseto

Ufadhili wa mesto ni utofauti wa njia mbalimbali za ufadhili na ni mkakati mwingine muhimu wa kuboresha ufadhili unaoongozwa na jamii kwa ajili ya usafi mazingira [24], haswa linapokuja suala la uendelevu wa kifedha katika chungu chetu. Ili MCSFF iweze kukuwa, kuna haja ya kufanya zaidi ya kuweka kianzio kwenye mfuko na kuuzungusha. Ikiwa ni pamoja na vyanzo vingine vya ufadhili, ambavyo vinaweza kuwa vya nje na vya ndani, vitaongeza uaminifu na kuruhusu ukuaji [24] Vyanzo vya fedha vya nje.

**Vyanzo vya fedha vya nje**

Linapokuja suala la njia za ufadhili wa nje, hizi kwa kawaida hutoka kwa wadau kama vile wafadhili binafsi, serikali za mitaa, na taasisi rasmi za kifedha. Ushirikiano na wafadhili binafsi na taasisi rasmi za kifedha zimekuwa na jukumu kubwa katika uendeshaji wa fedha ngazi za chini. Kwa mfano, AMT ilijenga ushirikiano na Benki ya Standard, ambao walikubali kutoa huduma za kufungua na kusimamia akaunti kwa wanachama wa vikundi vya kuweka akiba na kutoa mikopo kwa viwango vya kibiashara [21]. Mara nyingi wadau wenye nguvu zaidi, serikali za mitaa zinaweza kutoa msaada wa kifedha kwa kutoa ruzuku kutoka kwa bajeti za umma au kwa kujumuisha miradi katika mpango mkuu wa jiji, na kutoa huduma kwa njia mbadala za kifedha [25].

Mkakati wetu wa kwanza juu ya utawala unakamilisha mkakati huu wa pili. Kuwa na mfumo mzuri wa usimamizi wa fedha unaoimarisha uwajibikaji wa kifedha ni sehemu muhimu ya kuongeza kasi. Weru et al. [20-21] alishauri kwamba serikali na wawekezaji wanapendelea kufanya kazi na washirika ambao wameweka mbinu bora za kifedha, mipango ya usimamizi wa hatari na mifumo inayoweza kufuatiliwa ya ufuatiliaji na tathmini.

**Vyanzo vya fedha vya ndani**

Kupanua wigo wa vyanzo vya fedha kupitia rasilimali za ndani kunaweza kujumuisha hitaji la viwango vya riba na kuanzishwa kwa fursa za kuzalisha mapato. Kwa upande wa zamani, pia kuna usawa mzuri ambao lazima udumishwe na viwango vya riba. Mashirika ya mikopo midogo midogo ndani ya nchi tayari yanachukuliwa kuwa "wanyonyaji damu" na wakazi wengi kwa sababu ya viwango vya juu vya riba na mahitaji ya dhamana ya mali au wadhamini endapo kutakuwa na kasoro za mkopo [26]. Kwa hivyo, fedha zinazowalenga maskini wa mijini zinapaswa kutoa viwango vya riba ambavyo ni vya chini kuliko taasisi za mikopo midogo midogo au taasisi nyingine za benki ili kuvutia na kufikiwa, lakini kutokuwa na riba si jambo halisi.

Wakizungumzia uwezekano wa kupata mapato kutokana na huduma za usafi wa mazingira, zaidi ya washiriki kumi kati ya washiriki kumi na tisa katika warsha na wakazi wa Mabatini walionyesha nia ya kujenga vyoo vya jumuiya katika maeneo ya umma. Kutoza ada za watumiaji wa vyoo vya jumuiya katika maeneo haya ni uwezekano ambao ulipendekezwa na jamii. Hii inakuja na changamoto zake, kama inavyoonekana katika Mfano wa Uchunguzi 2 kutoka kwa Akiba Mashinani nchini Kenya. Kulipia matumizi ya vyoo kunaweza kuwa vigumu kwa wakazi wengi, na utunzaji wa vyoo vya jumuiya unaweza kupuuzwa kama utaratibu haujapangwa ipasavyo, na kusababisha changamoto zaidi za usafi wa mazingira [27]. Ukweli huu ulidhihirika katika warsha iliyopita na jamii, ambapo baadhi ya wenyeji walionyesha wasiwasi wao juu ya usimamizi na uwezo wa vyoo vya jumuiya katika makazi kama Mabatini.

**Mfano Uchunguzi 2:** Ilmeripotiwa kutoka kwa mfano wa utafiti wa AMT ya nchini Kenya kwamba kaya nyingi hazina vyoo majumbani mwao, na hivyo kusababisha kutumia vyoo vya jumuiya vya watu kibinafsi au katika maeneo ya umma. Vyoo hivi vya jumuiya hugharimu KSh 5 kwa mtu mzima na KSh 3 kwa mtoto (US$ 0.48/0.29). Kwa sababu vyoo hivi kwa kawaida ni vyoo vya mashimo, vinajaa haraka na vinahitaji kunyonywe mashimo na matengenezo ya mara kwa mara.

Matokeo yake, watu binafsi mara nyingi huamua kutumia mbinu mbadala kama vile makopo na mifuko ya karatasi, pia inajulikana kama "vyoo vya kuruka", kwa sababu ya gharama kubwa na hali isiyoridhisha ya vyoo. Zoezi hili linahusisha kutupa kinyesi kibichi juu ya paa au kwenye mifereji ya maji, na kusababisha matatizo zaidi ya mazingira na usafi wa mazingira. Hii haimaanishi kwamba vyoo vya jumuiya havipaswi kujengwa, lakini kwamba matengenezo na ufikiaji lazima izingatiwe katika kupanga [21].

## 2.3 Mkakati wa 3 - Jukwaa la chaguzi

Utaratibu wa ufadhili unaoongozwa na jamii, lazima uzingatie wigo mpana wachaguzi mahususi kushughulikia mahitaji mbalimbali ya vyoo na usafi wa mazingira ya jamii. Lazima kuwe na utambuzi wa mahitaji na haki za wanawake, wasichana, watu wanaoishi na ulemavu, na makundi mengine yaliyotengwa, na ushirikishwaji wao katika utoaji wa huduma za safi wa mazingira [6,28]. Zaidi ya hayo, ili kutoa mahitaji mbalimbali ya usafi wa mazingira ndani ya Jamii, ni muhimu kwenda zaidi ya mipaka ya mazoea ya kawaida ya kupanga. Uelewa wa kina wa eneo husika ni muhimu ili kuhakikisha kuwa fedha zilizokusanywa katika MCSFF zinatumika ipasavyo kushughulikia mahitaji mbalimbali. Aidha, hii pia itazuia masuluhisho yanayotokana na mfuko wa Akiba kuwa ya kizamani.

Kutokana na utafiti tulioufanya eneo la utafiti, MWAUWASA imeonyesha kutambua matatizo ya jamii, hata hivyo, mtazamo wa shirika hilo katika huduma za usafi wa mazingira jijini Mwanza ni katika ujenzi wa vyoo vya mtu binafsi ni mdogo. Hii ni kwa sababu utoaji wa vyoo vya mtu binafsi unahitajika ili kuwezesha upanuzi wa mpango wa SSS wa shirika. Kwa hivyo, ukosefu wa huduma za usafi wa mazingira kwenye makazi unazidisha wasiwasi. Kwa mfano, ndani ya makazi ya Mabatini, kuna kimoja tu cha choo cha umma kilichoboreshwa, ambacho kiko shuleni. Wasiwasi huu ulielezwa wakati wa warsha ya mwisho na jamii, huku wengi wakidai vyoo vingi vya umma katika maeneo yenye msongamano mkubwa kama vile masoko, maeneo ya ibada, na maeneo yenye watu wengi katika makazi hayo. Aidha, kutokana na matembezi tuliyofanya ndani ya mtaa na mahojiano mbalimbali, baadhi ya watu walieleza kuwa wamechukua mikopo kwa ajili ya malipo ya maji taka na kuunganisha maji safi, jambo ambalo linaonyesha hitaji la huduma nyingine za usafi wa mazingira zaidi ya kibanda cha vyoo cha mtu binafsi.

Hii ina maana kwamba pamoja na mpango uliopo wa upanuzi wa SSS wa MWAUWASA, ni muhimu pia kuchunguza jinsi MCSFF inavyoweza kufadhili miradi ambayo imeandaliwa kulingana na mahitaji ya eneo husika na inayoendeshwa chini ya uangalizi wa jamii ili kutoa masuluhisho yanakidhi mahitaji na endelevu ya usafi wa mazingira [29].



**Kielelezo cha 7:** Majadiliano ya Kikundi yaliyofanyika Gedeli, Mwanza, Tanzania, 2023. Picha: Ka Hei Chan

A Jalada la chaguzi linapaswa liangalie zaidi ya usawa wa usambazaji. Hii ina maana kwamba suluhisho hazipaswi kuzingatia tu uwepo au kutokuwepo kwa vyoo vya mtu binafsi au upanuzi wa mtandao wa SSS, badala yake, zinapaswa kutayarishwa kwa kushirikiana na jamii kwa kutekeleza mbinu shirikishi. Kulingana na Cairns Smith et al. [29], jalada la chaguzi linahitaji kuendelezwa kuelekea mkakati wa usawa wa huduma za usafi wa mazingira ambao unajumuisha mifumo midogo midogo iliyo nje ya mtandao wa maji taka, ambayo inaweza kubadilika kulingana na hali ya eneo. Zaidi ya hayo, utambuzi wa haki za mtu binafsi, utambulisho wa pamoja, na mahitaji maalum, hasa kwa wanawake, wasichana, watu wanaoishi na ulemavu, na makundi yaliyotengwa inapaswa kuwa mstari wa mbele katika mkakati huu [30].

Mfano wa uchunguzi 3 hapa chini unatoa mfano wa kile ambacho kutoa jalada la chaguo kunaweza kufikia

Hatimaye, jalada la chaguzi lazima pia lijumuishe uelewa wa maono ya muda mrefu ya kupanga kwa ajili ya makazi ili kupunguza hatari zinazoweza kutokea, kama vile zinazohusishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na majanga ya asili, na pia kukabiliana na mahitaji ya jamii ya siku zijazo [4]. Kwa sababu hizi, ushirikiano mkubwa kati ya jamii, serikali ya mtaa, na mamlaka ya maji unahitajika ili kuhakikisha kwamba jalada la chaguzi linaunga mkono maono ya muda mrefu ya jiji kwa ufanisi.

**Mfano Uchunguzi 3:** Usafi wa Mazingira Jumuishi wa Jiji (CWIS) ni mfumo ambao umezidi kuwa maarufu, na kutumika kati ya mamlaka za umma, watunga sera, benki za maendeleo na taasisi za kimataifa, kama vile Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Mfumo huo unalenga kuhakikisha usawa wa huduma za usafi wa mazingira na salama kwa wakazi wote wa mijini, wakiwemo maskini wa mijini. Ili kufanya hivyo, CWIS inasisitiza haja ya huduma za bei nafuu na zinazoweza kufikiwa ambazo hazizuiliwi na umiliki wa ardhi au aina ya vifaa. Hii inaashiria dhamira ya kuweka jalada la chaguzi wazi huku tukihakikisha usaidizi sawa wa kifedha kwa mahitaji maalum, ambayo ina maana kwamba mamlaka za huduma zinaweza kupeleka mbinu mbalimbali za kupanga kufikia makundi mbalimbali ya wateja ndani ya jiji. Ikilengwa kwa maeneo yenye maji taka na yasiyo na maji taka sawa, CWIS inalenga kupata matokeo ya wazi ya huduma kwa wakazi wote. Mfumo huo pia unajumuisha usawa wa kijinsia na kijamii kwa kuhusisha makundi yaliyotengwa katika michakato ya kufanya maamuzi na kulinda haki na afya za wafanyakazi wa usafi. Kwa kutekeleza kanuni hizi, CWIS inalenga kuanzisha mfumo endelevu na jumuishi wa usafi wa mazingira wa mijini ambao unakidhi mahitaji mbalimbali ya wakazi wa mijini huku ikihakikisha usaidizi sawa wa kifedha kwa watu maskini zaidi [31].



**Kielelezo cha 8:** Warsha ya Utayarishaji wa pamoja iliyofanyika Mabatini, Mwanza, 2023. Picha: Warda Reggane

## 3. Hitimisho

Ili chungu kiendelee kupika " katika fedha zinazozunguka, usawa katika kanuni za ushirikishwaji wa kijamii, uendelevu wa kifedha na muktadha wa mahali lazima udumishwe. Jijini Mwanza, na mazingira kama hayo, hili linaweza kukamilishwa kupitia mikakati kama vile kubuni mifumo thabiti ya usimamizi na utawala bora, vyanzo mbalimbali vya ufadhili, na kuwasilisha msururu wa chaguzi kwa wale wanaopata mfuko.

Kanuni na mikakati hii itaimarisha taratibu za ufadhili wa ngazi ya chini lakini kwa mfukokama vile MCSFF kuwa endelevu na kupanuka, ni lazima pia isingizwe katika mbinu shirikishi ya ufadhili. Maoni ya jumuiya ya wenyeji na ushiriki wa maana kutoka kwa walengwa unaweza kuhakikisha ushiriki wao wa dhati katika kusaidia miradi kama hii katika siku zijazo. Hata hivyo, wakati jumuiya ina jukumu kubwa la kutekeleza katika usimamizi na uhamasishaji, wao sio vyama pekee wanaohusika na hawawezi kubeba mzigo peke yao [32].

Kuna watendaji wengi wa ndani ambao tayari wanashiriki katika MCSFF na kuhakikisha ushirikiano wa haki na uliofafanuliwa vizuri. Ufadhili wa pamoja ni ufunguo wa sio tu kotofautisha ufadhili na kugawanya majukumu, lakini pia kujenga ushirikiano wa muda mrefu kati ya watendaji wakuu wa Mwanza ambao unaweza kutumika hata nje ya miradi ya usafi wa mazingira. Inasemekana kuwa msaada endelevu wa kifedha wa mradi mara nyingi hutegemea ushirikiano mzuri kati ya wadau wa ndani na wa nje [19]. Kwa sasa, uongozi wa aina hiyo wa jiji bado haupo jijini Mwanza kwa vile ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi haujaanzishwa kabisa.

Usafi wa mazingira salama na unaoweza kufikiwa ni haki muhimu ya binadamu [33] ambayo haipaswi kuangukia mtu binafsi kubeba mzigo wa kutatua peke yake [32]. Kwa hivyo, kila moja ya mikakati iliyopendekezwa katika muhtasari huu inazingatia na inasisitiza ufadhili wa pamoja. Kuanzisha miongozo ya wazi ya utawala bora na usimamizi hurahisisha ushirikiano wa uaminifu na uwajibikaji wa pamoja kati ya watendaji. Ufadhili wa pamoja ni sehemu muhimu ya ufadhili wa mseto, kwa sababu akiba za wana jamii haitatosha kukidhi mahitaji ya usafi wa mazingira, na kwa sababu kufadhili huduma muhimu haipaswi kuwa jukumu la walengwa peke yao. Hatimaye, kuwa na mibadala ya chaguzi kunasisitiza kwamba suluhu za ufadhili lazima ziongozwe na jamii lakini pia ionyeshe jukumu la serikali za mitaa katika kuunganisha miradi katika maono ya muda mrefu ambayo hayajatengwa na jiji lote.

Ni kupitia ufadhili wa pamoja pekee unaojumuisha kanuni muhimu za ujumuishaji wa kijamii, uendelevu wa kifedha na muktadha wa eneo halisi ambapo fedha kama vile MCSFF zinaweza kuongezeka na kuendelea kuzunguka kwa njia ya haki.


## Shukrani

Timu yetu ingependa kutambua mchango muhimu wa watu wengi waliofanikisha utafiti na sera yetu. Tungependa kuwashukuru washiriki wa timu yetu jijini Mwanza, Mussa Raido, Nadine Coetzee, na Aishath Green kwa juhudi zao na mchango wao muhimu katika mradi huu. Shukrani za pekee pia ziwaendee Mary Rubelwa, Festo Makoba, Tim Ndezi, Francis Reffell, na Daniel Mukeba kwa kutushirikisha uzoefu na utaalam wao. Hatimaye, tungependa kutoa shukrani zetu za kina kwa Profesa Adrianna Allen, Dkt. Rita Lambert, na Dkt. Pascale Hofmann kwa mwongozo wao na mchango wao wa busara kwa muda wote.

# Marejeleo


[1] Chow W, Singh C, Thomas A, Catt D, Chu E, Solecki W, et al. CSCPPM2 Cities and Settlements by the Sea. 2022

[2] Zhang J, Chen SS, Gao Q, Shen Q, Kimirei IA, Mapunda DW. Morphological characteristics of informal settlements and strategic suggestions for urban sustainable development in Tanzania: Dar es Salaam, Mwanza, and Kigoma. Sustainability (Switzerland). 2020 May 1;12(9).

[3] Gladys H, Tekalign T, Joyce N, Cecilia U. Youth-Led Mwanza City Informal Settlements Baseline State of Living Conditions and Access to Urban Basic Services. 2018: 1.

[4] Hambati H. Weathering the storm: disaster risk and vulnerability assessment of informal settlements in Mwanza city, Tanzania. International Journal of Environmental Studies. 2013; 70(6): 919–39.

[5] OVERDUE. About OVERDUE [Internet]. OVERDUE. 2020 [cited 2023 Jun 16]. Available from: https://overdue-justsanitation.net/?page_id=18

[6] Advancing just sanitation across urban Africa: Focus on Mwanza (Tanzania) MSc in Environment and Sustainable Development 2022/23-DEVP0022 Terms of Reference. 2022. From: https://overdue-justsanitation.net/?page_id=540#our_team_mwanza.

[7] Manga M, Bartram J, Evans BE. Economic cost analysis of low-cost sanitation technology options in informal settlement areas (case study: Soweto, Johannesburg). Int J Hyg Environ Health. 2020; 223(1): 289–98.

[8] Salim A. LVWATSAN-Mwanza Immediate Investent Plan (IIP) Environmental and Social Management Plan (ESMP) for Simplified Sewerage and Sewer Rehabilitation and Extensions in Ilemela and Nyamagana Districts-Mwanza Region. Mott Macdonald. 2016: VI-8.om

[9] UCL – University College London. OVERDUE: Tackling the sanitation taboo across Urban Africa. 2020. From: https://www.ucl.ac.uk/sustainable-development-goals/case-studies/2020/oct/overdue-tackling-sanitation-taboo-across-urban-africa

[10] Yap C, Mcfarlane C, Ndezi T, Makoba FD. Sanitation challenges in Dar es salaam: the potential of Simplified Sewerage Systems. Environ Urban. 2023: 13.

[11] Sheuya SA, Burra MM. Tenure Security, Land Titles and Access to Formal Finance in Upgraded Informal Settlements: The Case of Dar es Salaam, Tanzania. CUS. 2016;04(04):440–60.

[12] Dennis D. People and Systems for Water, Sanitation and Health: Water and sanitation services to the urban poor. 27th WEDC Conference. 2001: 253.[9] Tufvesson A, Bunduki A, Butoto L, Mkare D. Sustaining HESAWA in Mwanza region, Tanzania.

[13] Tufvesson A, Bunduki A, Butoto L, Mkare D. Maximizing the Benefits from Water and Environmental Sanitation: Sustaining HESAWA in Mwanza region, Tanzania. 31st WEDC International Conference. Loughborough University. 2005: 262-265.

[14] Cotton M, Motta BH. Engaging with environmental justice: governance, education and citizenship. Inter-Disciplinary Press. 2011: 270.

[15] Wamuchiru E. Beyond the networked city: situated practices of citizenship and grassroots agency in water infrastructure provision in the Chamazi settlement, Dar es Salaam. Environ Urban. 2017; 29(2): 551–66.

[16] CCI. CCI Tanzania | Urban Poor Fund (JENGA) [Internet]. n.d. [cited 2023 Jun 16]. Available from: https://ccitanzania.org/urban-poor-fund-jenga

[17] Trémolet S, Mansour G, Muruka G. Developing microfinance for sanitation in Tanzania. SHARE Research Consortium. 2015: 26-27.

[18] Ibrahim S. How to Build Collective Capabilities: The 3C-Model for Grassroots-Led Development. J Human Dev Capabil. 2017; 18(2):197–222.

[19] Carlsson L, Berkes F. Co-management: Concepts and methodological implications. J Environ Manage. 2005; 75(1): 65–76.

[20] Weru J, Njoroge P, Wambui M, Wanjiku R, Mwelu J, Chepchumba A, et al. The Akiba Mashinani Trust, Kenya: role of a local fund in urban development. International Institute for Environment and Development. 2017: 2-6.

[21] Weru J, Okoyo O, Wambui M, Njoroge P, Mwelu J, Otibine E, et al. The Akiba Mashinani Trust, Kenya: a local fund's role in urban development. Environ Urban. 2018; 30(1): 53–66.

[22] Alexandra B. Grassroots organizations are just as important as seed money for innovation. United Nations High Commissioner for Refugees. 2023: 1-4

[23] Oino P, Luvega C. The Dilemma in Sustainability of Community-based Projects in Kenya. Global Journal of Advanced Research. 2015; 2(4): 757-768

[24] WASTE Foundation. Financial Inclusion to Improve Sanitation & Health: A multi-stakeholder partnership addressing supply & demand sides of the global sanitation challenge. United Nations. 2023. From: https://sdgs.un.org/partnerships/financial-inclusion-improve-sanitation-health-multi-stakeholder-partnership-addressing

[25] International Federation of Accountants. Greater Transparency and Accountability in the Public Sector. 2022. From: https://www.ifac.org/what-we-do/speak-out-global-voice/points-view/greater-transparency-and-accountability-public-sector

[26] Wondirad HA. Interest rates in microfinance: What is a fair interest rate when we lend to the poor? Qual Quant. 2022; 56(6): 4537–48.

[27] Simiyu S. Determinants of usage of communal sanitation facilities in informal settlements of Kisumu, Kenya. Environ Urban. 2016; 28(1): 241–58.

[28] Colin Mcfarlane. Sanitation in informal settlements: a networked problem. International Institute for Environment and Development. 2015. From: https://www.iied.org/sanitation-informal-settlements-networked-problem

[29] Sarah Cairns Smith, Haley H, Emmanuel N. Urban Sanitation: Why a portfolio of solutions is needed?. The Boston Consulting Group. 2014: 16-18

[30] Rusca M, Alda-Vidal C, Kooy M. Sanitation justice? The multiple dimensions of urban sanitation inequalities. In: Water Justice. Cambridge University Press. 2018: 210–25.

[31] Schrecongost A, Pedi D, Rosenboom JW, Shrestha R, Ban R. Citywide Inclusive Sanitation: A Public Service Approach for Reaching the Urban Sanitation SDGs. Front Environ Sci. 2020; 28: 8.

[32] Otsuki K. Infrastructure in informal settlements: co-production of public services for inclusive governance. Local Environ. 2016; 21(12): 1557–72.

[33] United Nations. Human Rights to Water and Sanitation. 2023. From: https://www.unwater.org/water-facts/human-rights-water-and-sanitation



**Kwa taarifa zaidi wsiliana na:**
**Adriana Allen (a.allen@ucl.ac.uk),**
**Tim Ndezi (ccitanzania@gmail.com) au**
**Wilbard Kombe (kombewilbard18@gmail.com)**